

# Sambaza Upendo wa Mungu



Na Allie B., miaka 12, Kentucky, Marekani

Mimi na familia yangu tuliamia Kentucky muda mfupi uliopita. Nilikuwa mwenye huzuni sana kwa sababu nilikuwa nawaacha marafiki zangu wote na jamaa zangu. Kentucky palikuwa ni paha-li tofauti sana na kule nilikozoea. Kwa mara ya kwanza tulipoenda kanisani, niliona kwamba hakukuwa na watu wengi. Wakati nilipotambua ni kwa kiasi gani tawi langu lilikuwa dogo, niliamua kwamba badala ya kufikiria viba-ya kulihusu, ningefanya kitu kulihusu.

Siku iliyofuata, mimi pamoja na mama yangu tuli-kwenda dukani. Kabla hatujaondoka nyumbani, nili-chukua bunda la kadi. Tulipofika dukani, nilichukua peremende na kwenda kulipia. Keshia alipitisha pere-mende kwenye mashine, kisha akanipa. Nilimrudishia. Alionekana kuchanganyikiwa na akasema, “umekwisha ilipia, ma’am.”

Nikasema, “Najua, lakini ninakupa hii kama zawadi.” Kisha nikampa na kadi pamoja na peremende. Alitabasa-mu na kunishukuru. Aliangalia nyuma ya kadi, ambapo nilikuwa nimeandika “Kila mmoja ni mtoto wa Mungu.” Niliondoka nikiwa na furaha, nikijua kwamba hata kama hakujunga na Kanisa, bado nilifanya kitu kizuri.

Baadae siku hiyo, nilikumbuka kwamba nilikuwa nimeacha kadi zilizobaki kwenye meza ya keshia! Wakati mwingine tulipoenda dukani, nilikwenda kuuliza kama bado zilikuwa pale. Kisha niliona kitu, nikasimama. Karibu meza tano za makeshia zilikuwa na kadi zilizosema “Kila mmoja ni mtoto wa Mungu.” Keshia alikuwa amezigawa. Nilihisi furaha kwa kile nilichokifanya. ■

